# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MAJI
## WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KATIKA MRADI WA IGENGU, ILONGO, KIDARAFA, GUMANGA, MKALAMA, MWANDO, MARERA NA KIKHONDA**

**20.01.2020**

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI KWA KUSHIRIKIANA NA JUMUIYA ZA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII WANAWATANGAZIA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:**

### 1: FUNDI BOMBA WA JUMUIYA (NAFASI 8)

**Sifa za muombaji**

i. Awe na cheti cha kidato cha nne.
ii. Awe na cheti cha ufundi bomba grade one, two, level au diploma.
iii. Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kwenye kazi za miradi ya maji
iv. Awe na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kusimamia mafundi wasaidizi.
v. Awe na umri kuanzia miaka 18-45
vi. Awe ni raia wa Tanzania
vii. Awe na utayari wa kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Meneja.

**MAJUKUMU YA FUNDI BOMBA WA JUMUIYA**

1. Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa Jumuiya ya huduma ya maji katika ngazi ya jamii na Katibu katika Kamati ya huduma ya maji ngazi ya jamii
2. Kusimamia, kutekeleza na kufuatilia shughuli zote za uendeshaji wa mradi katika eneo husika la huduma
3. Kusimamia na kufuatilia ratiba zote za kazi walizo pangiwa Timu ya uendeshaji wa mradi (akiwemo Mhasibu, Operator na Mlinzi) na kushirikiana nao kwa vitendo.
4. Kushauriana katika masuala ya kiufundi na Meneja wa RUWASA Wilaya.
5. Ni kiungo kati ya Timu ya uendeshaji na Kamati ya huduma ya maji ngazi ya jamii
6. Kupokea maelekezo yote ya kiutendaji kutoka kwa Meneja wa RUWASA Wilaya
7. Atawajibika kutoa taarifa zote za kiutendaji kwa Meneja wa RUWASA Wilaya kwa kadiri atakavyo elekezwa
8. Atatoa taarifa za kiutendaji kwa kamati ya huduma ya maji ngazi ya jamii kadiri ya mwongozo

**2: MHASIBU WA JUMUIYA (NAFASI 8)**

**Sifa za muombaji**

- (i) Awe na cheti cha kidato cha nne/sita
- (ii) Awe amehitimu masomo ya fani ya Uhasibu kwa ngazi ya Astashahada (Certificate) au stashahada.
- (iii) Awe na umri kuanzia miaka 18-45.
- (iv) Awe na uwezo wa kuandaa taarifa za fedha.
- (v) Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta
- (vi) Awe mwadilifu
- (vii) Awe ni raia wa Tanzania,
- (viii) Awe na utayari wa kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Meneja.

**MAJUKUMU YA MHASIBU WA JUMUIYA**

1. Kusimamia ukusanyaji wa Ankara za malipo ya maji.
2. Kusimamia wauza maji katika vituo vya kuuzia maji na kukusanya fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya maji katika vituo.
3. Kufanya malipo yote baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Jumuiya ya huduma ya maji ngazi ya jamii na Meneja wa RUWASA Wilaya.
4. Kuandaa mpango wa mapato na matumizi ya kila mwezi na kutoa taarifa ya mapato na matumizi kila mwisho wa mwezi.
5. Kushauriana na Msimamizi wa Jumuiya katika masuala yahusuyo fedha katika kutekeleza shughuli za mradi.
6. Kutunza vitabu vya fedha, hati za malipo na nyaraka zote za uthibitisho wa mapato, malipo na matumizi ya fedha katika shughuli husika.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI HAYA YAFUATAYO**

1. Maombi yote yaambatane na vivuli vya vyeti vya masomo na mafunzo.
2. Muda wa kuleta maombi ni ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya Tangazo hili, siku ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **03 Februari, 2020** saa 9.30 Alasiri.
3. Waombaji wote waweke namba zao za simu kwenye barua za maombi, majibu yatatolewa kwa njia ya simu kwa wote watakaoitwa kwenye Usaili.
4. Waombaji wenye anuani za Barua Pepe (E-mail) na Fax waweke pia namba za simu katika barua zao za maombi, zitakazotumika kuwapatia majibu ya kuitwa kwenye usaili.
5. Waombaji waweke pia picha moja ya Passport Size ya rangi iliyopigwa hivi karibuni katika barua zao za maombi ya kazi.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na ziwasilishwe kwa;

**Meneja wa RUWASA,**
**S.L.P. 60,**
**SINGIDA.**
Au barua pepe**:** mkalamadm@ruwasa.go.tz

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**
**MENEJA WA RUWASA – MKALAMA**